TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

TAARIFA YA KAIMU MKURUGENZI WA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA (TEWW), DKT. KASSIMU NIHUKA KWA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA MHE. PROF.JOYCE NDALICHAKO (MB), KWENYE UZINDUZI WA BARAZA LA USIMAMIZI LA TEWW TAREHE 07/08/2018, DAR ES SALAAM.

TAARIFA YA KAIMU MKURUGENZI WA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA (TEWW), DKT. KASSIMU NIHUKA KWA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA MHE. PROF.JOYCE NDALICHAKO (MB) KWENYE UZINDUZI WA BARAZA LA USIMAMIZI LA TEWW TAREHE 07/08/2018, DAR ES SALAAM.

Mheshimiwa Waziri wa Elimu,Sayansi na Teknolojia Mh, Prof.Joyce Ndalichako (MB),

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Katibu Mkuu Mstaafu, Dkt. Naomi Katunzi,

Wajumbe wa Baraza la Usimamizi la TEWW,

Wajumbe wa Menejimenti ya TEWW,

Waandishi wa habari,

Mabibi na mabwana.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa niaba ya jumuiya ya Wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ninayo furaha kubwa kukukaribisha rasmi wewe binafsi pamoja na wageni wote ulioambatana nao hapa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika hafla hii ya uzinduzi wa Baraza la Usimamizi la TEWW. Ninatambua kuwa unayo majukumu mengi ya kitaifa, lakini umeweza kutenga muda wa kuja kuzindua Baraza la Usimamizi la TEWW. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri,

Kama unavyofahamu, TEWW ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 12 ya mwaka 1975. TEWW ina ofisi katika mikoa 21 kati ya 26 ya Tanzania Bara na ina Kampasi tatu (03) katika mkoa wa Dar es salaam, Morogoro na Mwanza.

Pia TEWW ina jumla ya wafanyakazi 252 kati yao wanataaluma 86 na waendeshaji 166.

Pamoja na majukumu mengine, TEWW ina majukumu yafuatayo:

(i) Kuandaa programu na kutoa mafunzo kwa walimu na waendeshaji wa elimu ya watu wazima;
(ii) Kutoa mafunzo kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa;
(iii) Kutoa elimu kwa umma na kuendesha mafunzo ya kisomo;
(iv) Kuandaa mitaala, mihtasari na machapisho kwa ajili ya elimu ya watu wazima;
(v) Kuendesha mitihani na kutoa tuzo mbalimbali kuhusu elimu ya watu wazima;
(vi) Kuanzisha vituo vya mafunzo, ujifunzaji na utafiti;
(vii) Kuandaa na kufanya semina, warsha, makongamano na mafunzo ya muda mfupi kuhusu elimu ya watu wazima;
(viii) Kushirikiana na wadau katika kutoa elimu ya watu wazima na kuwaratibu.

Mheshimiwa Waziri,

Pamoja na mambo mengine, Baraza lililomaliza muda wake tarehe 03/04/2018, liliweza kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo kwa mafanikio makubwa:

(i) Kudurusu (review) Sheria Namba 12 ya mwaka 1975 ili iendane na dhima ya "Kujenga jamii inayojiendeleza";
(ii) Kuandaa Mpango Mkakati wa TEWW wa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2014/2015 mpaka 2018/2019 ambapo "review" imeanza na inaendelea;
(iii) Kuandaa sera, miongozo na sheria ndogo ndogo zinazoongoza utekelezaji wa majukumu ya TEWW. Katika kipindi hiki, TEWW imeweza kutengeneza Sera tano (5) ambazo ni Sera ya TEHAMA, Sera ya Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework), Sera ya UKIMWI, Sera ya

Utumishi na Sera ya Utafiti. Pia kupitia Baraza lililomaliza muda wake TEWW imeweza kuhuisha kanuni za mitihani na miongozo ya uandishi wa Makala na utwalii kwa wanataaluma;

(iv) Kuandaa Mkakati wa kuinua Kisomo na Elimu kwa Umma (National Literacy and Mass Education Strategy) ambao utekelezaji wake unaanza mwaka 2018/2019;

(v) Kuanzisha darasa la kisomo moja la mfano lenye wanakisomo 144 Wilayani Chamwino – Dodoma. Kati yao, 110 (76.4%) wana umri kati ya miaka 18 – 35 na wengine 34 (23.6%) wana umri wa miaka 36 na kuendelea. Tunategemea kundi la kwanza litamaliza mafunzo yake mwishoni mwa mwezi Agosti, 2018;

(vi) Kununua jumla ya mitambo 7 ya kiwanda cha uchapaji yenye thamani ya jumla ya Sh. 299,000,000/= zilizotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Napenda nikushukuru sana wewe binafsi pamoja na Wizara yako kwani mitambo hii imesaidia kuboresha utendaji kazi za kiwanda hasa katika uzalishaji wa moduli na majarida mbalimbali ya TEWW;

(vii) Kujenga kumbi mbili za mihadhara katika Kampasi ya WAMO- Morogoro zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360, kwa gharama ya Sh. 400,000,000/= (yaani 200,000,000/= kutoka fedha za ndani na 200,000,000/= kama mkopo kutoka TEA);

(viii) Kuweka viti vya kudumu 360 katika kumbi mbili za mihadhara (Kampasi ya WAMO- Morogoro) na viti 855 katika kumbi tano (Makao Makuu – Dar es Salaam);

(ix) Upanuzi wa utoaji wa programu za mafunzo ya elimu ya watu wazima kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada ambapo udahili uliongezeka

kutoka wanafunzi, 1,146 mwaka 2014/2015 hadi kufikia wanafunzi 4,500 mwaka 2017/2018; na

(x) Kuanzisha programu ya kuzuia mimba za utotoni inayotekelezwa katika Wilaya za Kongwa na Bahi (Dodoma) na Nkasi na Kalambo (Rukwa) kwa ufadhili wa "Commonwealth of Learning". Programu hii inalenga kuwajengea stadi za ufundi, ujasiriamali na elimu ya afya na jinsia wasichana walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kwa sababu ya mimba za utotoni;

Mheshimiwa Waziri,

Pamoja na mafanikio haya, TEWW imekuwa ikikabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Taasisi mikoani. Kwa sasa TEWW ina magari katika vituo vya mikoa saba (7)tu ikiwemo Makao Makuu – Dar es Salaam kati ya vituo vya mikoa 21. Aidha, tunashukuru Wizara yako kwa kutupatia gari moja katika mwaka wa Fedha 2017/2018.

(ii) Taasisi inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti unaosababisha TEWW kushindwa kuwafikia walengwa wengi nchini husasani kwa programu za stadi za ujuzi, ujasilia mali na elimu ya afya na jinsia;

(iii) Upungufu wa wafanyakazi 53 hasa katika vituo vya mikoa hususani katika kada ya wanataaluma, wataalamu wa TEHAMA, Watunza Kumbukumbu (Records) na madereva.

Mheshimiwa Waziri,

Kwa kushirikiana na Baraza utakalozindua leo, TEWW imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo;

(i) Kukamilisha kudurusu (review) ya Sheria Na. 12 ya TEWW ili ianze kutumika;

(ii) Kukamilisha "review" ya Mpango Mkakati wa TEWW kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 – 2022/2023;

(iii) Kutekeleza programu ya kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwa kuandaa na kutoa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya kisomo kwa kuandaa kampeni mbalimbali. Lengo ni kuwafikia wanakisomo 1,000 katika mikoa 10 ya awali (yaani wanakisomo 100 kwa kila mkoa). Jukumu hili linaendana na dhima ya TEWW ya "kujenga jamii ya watu wanaojiendeleza" na pia linaendana na Sheria Na. 12 ya mwaka 1975 na Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978;

(iv) Kuweka mifumo ya Kielektroniki kama vile "Learning Management System", Government electronic Payment Gateway na mingineyo ili kuongeza ufanisi na ubora wa huduma zetu pamoja na kuweka mfumo mpya wa umeme katika jingo la makao makuu ya TEWW;

(v) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa programu za Astashahada, na Stashahada kutoka 4,500 mwaka 2017/2018 mpaka 6,675 mwaka 2018/2019 na wanafunzi wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka 10,420 mwaka 2017/2018 mpaka 12,000 mwaka 2018/2019;

(vi) Kujenga ofisi ya mkoa wa Kagera na kukamilisha ukarabati wa madarasa katika kituo cha Moshi- Kilimanjaro;

(vii) Kuimarisha uwezo wa Maktaba ya TEWW kwa kuweka mifumo ya TEHAMA (automation) na kuongeza eneo la kujisomea (extension); na

(viii) Kufanya utafiti katika programu za elimu nje ya mfumo rasmi ili kubainisha hali ya sasa ya vijana na watu wazima wasio na stadi za kisomo na kupata taarifa mahsusi zakupanga mikakati ya kupambana na adui ujinga,

Mheshimiwa Waziri,

Mwisho kabisa, naomba kwa niaba ya Menejimenti ya TEWW, nikushukuru sana kwa kutupatia Mwenyekiti wa Baraza la Usimamizi pamoja na Wajumbe wake. Aidha, tunakushukuru sana kwa kutenga muda wako na kuja kuzindua Baraza la Usimamizi la TEWW leo hii. Na sasa kwa heshima na taadhima naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Baraza, Dkt. Naomi Katunzi ili aongee nasi na hatimaye akukaribishe uweze kutupa nasaha.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA